# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – UTUMISHI NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI (KRUB) KUHUSU BAJETI YA OFISI HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais- Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii pia kutoa salamu za rambi rambi kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ofisi ya Bunge, na familia ya Macha kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu marehemu Dkt. Elly Macha. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais – Utumishi na Utawala Bora, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani kwa nguvu zote

vitendo vinavyoendelea kutokea katika nchi yetu vya utekaji, utesaji na uuaji wa raia na polisi wasio na hatia hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** ni bahati mbaya sana kwamba, wakati matukio haya yanaendelea kutokea, Serikali nzima pamoja na vyombo vyake vya ulinzi na usalama, imekaa kimya na haijatoa tamko lolote juu ya jitihada zinazofanyika kukabiliana na matukio haya yanayoikumba nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa pia na kiti cha spika kilivyotumika vibaya kuzuia wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi na ambao baadhi yao wamelalamika kuwa wametishiwa maisha, kujadili jambo hilo kwa kujificha nyuma ya kivuli cha Kanununi za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa pia kuona Waziri anayehusika na Utawala Bora kukataa masuala yanayohusu utawala bora kujadiliwa Bungeni na kuongeza kwamba wanaolalamikia matukio ya utekaji na utesaji ni wachochezi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiasa Serikali kuacha kuzuia Bunge kujadili suala hilo vinginevyo wananchi wanaweza kufikiri matukio hayo ya utekaji na utesaji yanayoratibiwa na vyombo vya dola na ndio maana serikali inaona ugumu wa kutoa kauli kuhusu jambo hilo. Mheshimiwa Spika, tukio la kuuwawa kwa polisi wanane tarehe 14/04/17 liisukume Serkali kutoa tamko kuhusu Ulinzi na Usalama wan chi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna usemi usemao kwamba **"vyombo vya ulinzi na usalama vinapoilinda Serikali basi vinakuwa**

**adui wa wananchi"** na hicho ndicho kinachotokea sasa katika nchi yetu. Mtazamo wa kuilinda Serikali usipobadilika basi usalama upo mashakani, kwani ni dhahiri kwamba vyombo hivyo vinatagema taarifa toka kwa wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wahusika wajitafakari kwa amani ya nchi yetu.

## 2. SERIKALI YA AWAMU YA TANO INAVYOKIUKA MISINGI YA NA UTAWALA BORA

**Mheshimiwa Sika,** dhana ya utawala bora imejengwa katika msingi wa Katiba ya nchi inayoheshimu mgawanyo wa madaraka katika mihimili mikuu ya dola ,demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu na uhuru wa kutoa maoni na kupata habari, uhuru wa kukusanyika na kujiunga na mashirika au vyama mbalimbali katika jamii n.k Aidha, utawala bora una sifa za uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu usawa na kuzingatia taratibu za kisheria na kikanuni katiaka utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** tukijipima kama taifa, kwa maana hiyo ya utawala bora, na kwa sifa hizo za utawala bora utaona kwamba nchi yetu iko nyuma sana katika utekelezaji wa misingi ya utawala bora. Kwa mujibu wa hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2017 ni kwamba; matukio yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Serikali hii ya awamu ya tano ya kupiga

marufuku mikutano ya vyama vya siasa, Kupiga marufuku urushwaji wa moja kwa moja wa mijadala ya bunge kupitia vyombo vya habari, Kudhibiti wabunge na hasa wa upinzani kutoa mawazo yao kwa uhuru bungeni, kuingilia mhimili wa mahakama katika kuulekeza namna ya kufanya kazi yake, kupuuza utawala wa sheria kwa kuruhusu wahalifu kuuwawa na polisi bila utaratibu wa sheria kuchukua mkondo wake, na uonevu unaofanywa na vyombo vya dola dhidi ya wananchi wa visiwa vya unguja na pemba si tu yanavunja Katiba ya nchi yetu na misingi ya utawala bora, bali pia yanaidhalilisha nchi yetu katika medani za kimataifa.

### 2.1. Uwajibikaji wa Pamoja

**Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza hapo awali, dhana ya utawala bora ina sifa ya uwajibikaji wa pamoja. Tofauti na awamu zilizopita za utawala, Sifa hii muhimu ya utawala bora ya uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility) imeanza kupotea katika Serikali hii ya awamu ya tano.

**Mheshimiwa Spika,** nasema hivi kwa sababu tumeshuhudia kwa nyakati tofauti kauli zinazokinzana za serikali hiyo hiyo moja. Kwa mfano, matukio ya hivi karibuni la mkuu wa nchi kutengua hadharani agizo la aliyekuwa waziri wake wa Katiba na sheria juu ya sharti la kuwa na cheti cha kuzaliwa ili mtu aweze kufunga ndoa, waziri wa afya kutofautiana na makamu wa rais juu ya upungufu wa dawa na vifaa tiba nchini, mkuu wa nchi kupinga taarifa za njaa alizopewa na baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa, waziri wa ardhi

kupinga mchakato wa kumpatia ardhi mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na mengine yanayofanana na hayo ni ishara tosha kwamba kuna tatizo kubwa la mawasiliano na uwajibikaji wa pamoja katika Serikali hii. Aidha, ni dalili mbaya kwamba Serikali inaelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake, kutokana na kutokuwa na msimamo wa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba Serikali irudi katika misingi ya uwajibikaji wa pamoja ambao ni sifa muhimu ya utawala bora. Serekali izungumze lugha moja. Waziri mmoja anapotoa tamko, tamko hilo liwe ni kwa niaba ya Serikali nzima kwani kwa kutofanya hivyo Serikali itawachanganya wananchi. Aidha, Mkuu wa nchi awaache mawaziri wake wafanye kazi kwa kujiamini ili wawe na tija katika majukumu yao. Kuwaingilia kila wakati au kuwapinga hadharani kunawavunja moyo na kunawafanya wafanye kazi kwa woga wakihofia kutumbuliwa au kuumbuliwa.

## Usawa wa Jinsia na Ushirikishwaji katika vyombo vya Uamuzi

**Mheshimiwa Spika,** usawa wa jinsia na ushirikishwaji katika vyombo vya uamuzi ni miongoni mwa nguzo muhimu za utawala bora. kumekuwa na tatizo duniani la ushirikishwaji hasa wa wanawake katika vyombo vya maamuzi. Kutokana na hali hiyo kumekuwa na vuguvugu katika mataifa mbalimbali duniani ya kuhakikisha kuwa

wanaweke wanawakilishwa vya kutosha katika vyombo vya uamuzi ili kukidhi matakwa ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa bara la Afrika, vuguvugu la kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi lilipelekea nchi wananchama wa Jumuiya ya SADC kuazimia kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi angalau kufikia asilimia 50. Ibara ya 12 ya mkataba wa SADC inasema kwamba: ***"Parties shall endeavour that, 2015, at least fifty percent of decision-making positions in Public and Private sector are held by women including the use of affirmative action measures as provided for in article 5"***

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya SADC na iliridhia mkataba huo. Kulikuwa na jitihada za kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi hapa nchini katika Serikali ya awamu iliyopita lakini takwimu zinaonyesha kwamba nafasi za wanawake katika awamu hii ya tano zimepungua.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni kwamba, hadi kufikia Julai, 2016 uteuzi wa Baraza la Mawaziri ulionyesha kushuka kwa idadi ya wanawake ukilinganisha na kipindi cha Serikali ya awamu ya nne. Wakati serikali ya awamu ya nne iliteua mawaziri wanawake 10 sawa na asilimia 33.3 ya Baraza lote, Serikali ya awamu ya tano iliteua mawaziri wanawake wanne tu kati ya mawaziri 19 sawa na asilimia 21.1 na hivyo

kufanya uteuzi wa wanawake mawaziri kushuka kwa asilimia 12.2.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya TGNP inaonyesha pia kwamba, kati ya makatibu wakuu 29 walioteuliwa, 26 walikuwa ni wanaume sawa na asilimia 89.7 huku wanawake wakipungua kutoka watano sawa na asilimia 21.7 ya mwaka 2014 hadi kufikia watatu sawa na asilimia 10.3 kwa sasa, na hivyo kufanya uteuzi wa wanawake katika nafasi hizo kupungua kwa asilimia 10.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa wakuu wa mikoa, idadi ya wanawake imeshuka zaidi. Kati ya wakuu wa mikoa 26 ya Tanzania Bara, 21 ni wanaume sawa na asilimia 80 na wanawake ni watano tu sawa na asilimia mbili. Hali kadhalika idadi ya wakuu wa wilaya imezidi kuporomoka ikilinganishwa na awamu iliyopita. Hali hii ya kushuka kwa uteuzi wa wanawake inaonekana pia kwa nafasi za makatibu tawala wa mikoa na wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Tanzania ni kati ya mataifa duniani yaliyoridhia na kusaini mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayoweka misingi ya usawa kwa binadamu ikiwamo ushiriki katika ngazi zote za maamuzi, lakini haitekelezi mikataba hiyo. Mikataba hiyo ni pamoja na Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (UDHR: 1948), Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW: 1979),

Mpango kazi wa Beijing (1995), Mkataba wa Ziada wa Maputo na Mkataba wa Nyongeza wa Jinsia na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kwamba ni sera ya dunia ya kuhakikisha kwamba kuna ushirikishwaji (inclusiveness) katika ngazi za maamuzi kwa sababu makundi ya wanawak, walemavu nk yana mahitaji tofauti, hivyo uwakilishi wao ni muhimu sana. Aidha, Serikali itambue pia kwamba kundi la wanawake ndio kundi la uhakika la wapiga kura hivyo,

## 3.0. MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** Watumishi ni Rasilimali ya msingi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Serikali katika ngazi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla. Nguvu na mafanikio ya Taasisi yoyote na Taifa lolote inategemea aina ya watumishi waliopo kwenye Taasisi au Taifa husika. Kwa msingi huo hawana budi kuendelezwa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania 2010/11-2014 (MKUKUTA – II) uliopangwa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, unasisitiza suala la kujenga uwezo, weledi upangaji na matumizi mazuri ya Rasilimaliwatu kuwa ni moja ya njia

muhimu ya kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kimsingi utumishi wa umma hauwezi kuwa na watumishi bora wenye upeo wa kutekeleza majukumu yao kufikia malengo ya taasisi na taifa kama mafunzo hayatapewa kipaumbele

**Mheshimiwa Spika,** Kutoa mafunzo ni jukumu la msingi la serikali, hivyo kusomesha watumishi ni sawa na uwekezaji katika sekta ya barabara, afya na maji. Hivyo basi, Umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kuwa nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo. Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 unasisitiza kwamba:

i. Watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wapatiwe mafunzo elekezi ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa.
ii. Waajiri wote wahakikishe kwamba watumishi wapya wafanyiwe upekuzi kwanza na kupatiwa mafunzo elekezi yanayohusiana na majukumu yao.
iii. Waajiri wote wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya mafunzo haya.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya maelekezo ya waraka huo, katka Awamu hii tano, waajiri wamekuwa wakitenga bajeti kidogo au kutotenga kabisa kwa ajili ya mafunzo, hivyo

kutoa kipaumbele cha mwisho katika mipango na bajeti. Aidha, Programu za mafunzo zimekuwa haziendani na mahitaji kwa maana kwamba mafunzo yatolewayo hayamwandai mtumishi kuwa mbobezi katika kazi yake au kupanda ngazi na kupata madaraka zaidi. I

**Mheshimiwa Spika,** inasikitisha zaidi kwamba, hata pale mafunzo yanapotolewa, watumishi hushawishika kuacha kazi Serkalini kwa sababu ya mshahara kutolingana na ujuzi walioupata, mfumo usioruhusu mabadiliko yanayoendana na ujuzi mpya wa mtumishi na kukosekana kwa ushindani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba program ya mafunzo kwenye kila idara ipewe kipaumbele katika bajeti. Aidha, Serikali ipanue wigo wa mafunzo nje ya nchi kwani mazingira ya nje yanampa mtumishi *exposure* uzoefu wa kutazama mambo kwa namna tofauti. Vilevile, baada ya mafunzo, yawepo mabadiliko ya ngazi na majukumu yanayoendana na mafunzo mapya ya mtumishi

## 4. UTUMBUAJI WA WATUMISHI USIOZINGATIA SHERIA.

**Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, nilizungumzia kuhusu ukiukwaji wa sheria ya Utumishi wa Umma na 5 ya mwaka 2002 kuhusu utumbuaji wa watumishi usiozingatia taratibu za kikanuni na kisheria. Ukiukwaji huo bado unaendelea licha

ya kupingwa vikali na Tume ya Haki za Binadamu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** bado Mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya wameendelea kukiuka sheria hiyo kwa kuwafukuza kazi watumishi kiholela na mbaya zaidi wanafanya hivyo hadharani kwenye mikutano ya hadhara. Kambi rasmi ya Upinzani haipingi watumishi kuchukuliwa hatua za kinidhamu pale inapothibitika ni wakosaji lakini, hatua hizo zizingatie utaratibu wa sheria uliowekwa ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi ya kujieleza na kujitetea.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana utumbuaji holela, hofu imejengeka kwa watumishi, ari ya utendaji kazi imepungua, heshima ya utumishi wa umma imeshuka jambo ambalo limeshusha ufanisi katika utumishi wa umma. Watumishi wa umma hawana ubunifu tena, wala ujasiri wa kufanya maamuzi, kutokana na woga kwamba wanaweza kukosea halafu baadaye wakatumbuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kuzingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu katika kushughulikia nidhamu ya utumishi wa umma ili kujenga Utumishi wa Umma madhubuti, unaojiamini na unaozingatia haki na utawala wa sheria

## 5. USHIRIKI WA WATUMISHI WA UMMA KATIKA SIASA

**Mheshimiwa Spika,** ni dhana inayoeleweka kwamba utumishi wa umma unatakiwa kuwa '***neutral and impartial'***

(yaani usiwe na mrengo wowote wa kisiasa) na kwamba uwe tayari mara zote kutekeleza sera  za Serikali ya chama chochote kitakachoingia .

**Mheshimiwa Spika,** lengo la dhana hiyo, ni kuifanya sekta ya utumishi wa umma kuwa endelevu (stable) na kuepuka mabadiliko ya watendaji wakuu kila Serkali ya chama tofauti kinapoingia madarakani. **Mheshimiwa Spika,** Serikali hii ya awamu ya tano imekiuka dhana hiyo kwa kuingiza siasa katika utumishi wa umma. Katika awamu hii ya tano, tumeshuhudia nafasi za utendaji Serikalini zikitolewa  kwa Makada na wakereketwa wa CCM ambao baadhi hawana hata ufahamu wa uendeshaji Serkalini(Government Adminisration). Tumeshuhudia uteuzi wa Afisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye alikuwa bado kazini akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kasulu na baadaye kuenguliwa nafasi yake na kurudishwa Jeshini. Tumeshuhudia pia Naibu Katibu Mkuu wa Tume ya Mipango akigombea ubunge wa  Bunge la Afrika Mashariki huku  akiwa bado mtumishi wa ngazi ya juu Serkalini.

**Mheshimiwa Spika,** Idadi kubwa ya Wakurugenzi Watendaji 65 kati ya 195 walioteuliwa walikuwa wagombea wa ubunge  kwenye kura za maoni za CCM. Aidha, baadhi ya Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na Makatibu wakuu ni wakereketwa wa Chama cha Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya maamuzi ni  kuingiza siasa katika utumishi wa umma na kupoteza weledi "Proffessionalism" na ni kupanda mbegu mbaya ya ubaguzi

wa kisiasa katika utumishi wa umma. Inakuwaje kwa mfano, chama kingine kikichukua madaraka ya dola? Hali ya watumishi wenye itikadi tofauti itakuwaje? Je Naibu Katibu Mkuu wa Tume Mipango ambaye kura zake hazikutosha katika kugombea Ubunge wa Afrika Mashariki amerudi kazini? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiasa Serikali kuacha mara moja kuteua au kuajiri watumishi kutokana na itikadi za kisiasa. Aidha, Kambi Rasmi ya upinzani inaishauri Serkali ijenge, utumishi wa umma wenye weledi ambao uhai wake hautegemei Chama kilichopo madarakani, bali Utumishi wa Umma endelevu unaotumikia wananchi.

## 6. UHAKIKI WA WATUMISHI, AJIRA MPYA NA UJIRA WA WATUMISHI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilisitisha ajira mpya kwa maelezo kwamba ilikuwa ikifanya uhakiki wa watumishi. Hata hivyo, Serikali imeanza tena kutoa ajira mpya. Kambi Rasmi Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kama uhakiki umekamilika na ni kitu gani kilichogundulika katika uhakiki huo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na tatizo la ukosefu wa ajira kuendelea kukua katika nchi yetu, na kutokana na matukio ya utumbuaji holelea na mfumo wa uajiri usiotabirika, vijana wengi wa nchi hii waliofuzu masomo yao wameingiwa na hofu na kukata tama kwa kuwa hawajui kesho yao itakuwaje. Kutokana na hali hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe

inatoa Mpango wake wa ajira katika sekta mbalimbali kwa kila mwaka wa fedha ili watu wajue ni ajira ngapi zitatoka katika mwaka husika wa fedha. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezaa Bunge hili kuwa imepanga kutoa ajira ngapi katika mwaka wa fedha 2017/18?

**Mheshimiwa Spika,** licha ya umuhimu wa kuwa na mpango wa ajira unaotabirika, ujira wa watumishi nalo ni jambo la kuzingatia. Ujira una faida za aina mbili; kwanza unamtegemeza mtumishi kwa maana ya kipatoa ambacho atakitumia kujikimu, na kuendesha shughuli zake nyingine, lakini pili, ni chanzo cha mapato ya Serikali kupitia kodi ya mapato kwa watumishi (PAYE).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia hali hiyo, maboresho ya ujira kwa watumishi ni jambo la msingi sana. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Tume ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba ujira kwa mwezi kwa sekta zote za ajira, takriban asilimia 25.3 wanapokea kati ya shilingi 300,001/- na 500,000/- Asilimia 17.9 wanapokea kati ya shilingi 500,001/- na 1,500,000/-. Hivi ndivyo viwango vya mishahara ambayo watumishi wengi wanapokea na hawa ndio walipakodi wa uhakika wa nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya viwango hivi kwani haviendani na mpango wa maendeleo wa miaka mitano unaohitaji Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati.

**Mheshimiwa Spika,** maendeleo ni kwa watu na sio kwa vitu, na uchumi ambao sio shirikishi hauwezi kuwa ni uchumi endelevu. Naomba kunukuu kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba ***"You cannot develop people, you must allow people to develop themselves",*** hivyo ujira stahiki kwa kazi stahiki ndiyo nyenzo pekee ya kumletea Mtanzania maendeleo na si vinginevyo.

## 7. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS - MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

### 7.1. Menejimenti ya Utumishi wa Umma ( Fungu 32)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2016/17 Menejimenti ya Utumishi wa umma ilitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 30.341**, kati ya hizo shilingi bilioni 22.79 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.55 kwa ajili ya kutegeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi bilioni 16.338 sawa na 53.8% kati ya hizo shilingi bilioni 15.65 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 690 sawa na asilimia 9.14 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kiasa cha fedha za maendeleo zilizotolewa hadi Machi, 2017 haikidhi bajeti ya maendeleo katika Wizara . Kwa mwaka 2017/18 Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 32.578 ambalo niongezeko la shilingi bilioni 2.237 ukilinganisha na maombi ya mwaka uliopita. Kati ya maombi hayo shilingi bilioni 25.578 ni kwa

matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** fedha za maendelo zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni pungufu ya shilingi milioni 500.5 ukilinganisha na fedha za maendeleo za mwaka wa fedha 2016/17. Tafsiri ya kutotekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17asilimia 90, na tafsiri ya kushusha kiwango cha fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni kiashiria kwamba miradi ya maendeleo katika fungu hili sio kipaumbele na kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza fungu hili isitengewe kabiasa fedha za maendeleo kwa kuwa inaoneka kwamba fedha hizo hazina kazi.

### 7.2. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67)

**Mheshimiwa Spika,** Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma, ni taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Rais na inatekeleza majukumu mahususi kwa mujibu wa kifungu cha 29(4) na (6) cha sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 18 ya mwaka 2007, ikiwa na jukumu kuu na la msingi la kuwezesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Mabadiliko ya teknologia, yamegusa hata mchakato wa ajira duniani kote, kuna mabadiliko ya nyenzo bora zinazotumika kuweza kupata watumishi wenye

weledi na maadili, Hata hivyo bajeti ya Sekretariat ya ajira haikisi malengo ya mabadiliko hayo**.**

**Mheshimiwa Spika** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali, kutenga bajeti ya kutosha kuwezesha Sekretariati ya Ajira ili wafanye kazi kitaalam. Rasilmali watu ndio ingini ya Maendeleo bila kuajiri wataalam wananaofaa lengo la kufikia uchumi wa kati litakuwa ndoto.

### 7.3. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (fungu 33)

**Mheshimiwa Spika,** taasisi hii ina jukumu muhimu la kusimamia maadili ya viongozi wa umma na kufanya uchunguzi wa awali wa malalamiko kuhusu ukiukwaji wa maadili, na kufanya utafiti kuhusu hali ya uadilifu wa viongozi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu baadhi ya Viongozi kukiuka maadili ya Utumishi wa Umma km kiongozi kudai kwa nguvu mali za watu kwa njia zisizo halali, kumiliki mali nyingi kulinganisha na vyanzo vyake vya mapato, kuvamia ofisi za watu akiwa na askari ili kazi yake ipewe kipaumbele cha kwanza, kiongozi kufukuza na kuwadhalilisha watumishi wa umma hadharani bila ya kufuata utaratibu n.k. hizi zote ni changamoto ambazo zinatakiwa kutatuliwa. Hata hivyo, hatujawahi kusikia hatua ambazo zimechukuliwa na Tume hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serikali kwamba ili Tume hii iwe

huru bila ya kuingiliwa na kiongozi yeyote, Uteuzi wa mtendaji mkuu uthibitishwe na Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2016/17 Taasisi hii ilipangiwa kupata shilingi bilioni 5.914 lakini hadi mwezi March, 2017 fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 2.885 sawa na 49% kati ya fedha hizo, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 1.317 sawa na 52% ya matumizi ya kawaida. Taasisi hii kulingana na umuhimu wake wa kusimamia maadili ambalo ndio nguzo ya Utawala bora kwa bajeti hiyo bado ni kichekesho kutimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 Sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma inaomba kupewa kiasi cha shilingi bilioni 5.99 na matumizi mengineyo wanaomba shilingi bilioni 2.604. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa umuhimu wa Taasisi hii iliyopo Kikatiba kiasi hicho cha fedha ni kidogo katika kusimamia maadili ambayo ndio nguzo muhimu katika utawala bora.

## 8. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuendelea kusisitiza suala la Utawala Bora katika nchi yetu. Kitendo cha Idara ya Usalama wa Taifa kutuhumiwa kwamba inaratibu na kuendesha vitendo vya utekaji na utesaji wa raia wasio na hatia ili kutimiza maslahi ya kisiasa ya baadhi ya viongozi wa Serikali, sio jambo lenye afya katika mustakabali wa usalama na amani ya nchi yetu

iliyodumishwa kwa zaidi ya miaka 50. Aidha, kitendo cha Serikali kukanusha tuhuma hizo na kukataa kufanywa kwa uchunguzi juu ya jambo hilo kunaacha maswali mengi yanayohitaji kupatiwa majibu.

**Mheshimiwa Spika,** sisi ni viongozi ambao tuna jukumu la msingi la kujenga misingi ya utu, udugu na upendo kwa vizazi vijavyo ili taifa liendelee kuwa salama na amani. Ushabiki wetu katika kuzuia jambo hili la utekaji nyara, mauaji ya viongozi wa serkali za mitaa, lisifanyiwe uchunguzi ni kubariki na kuhalalisha matukio hayo yaendelee kufanyika hapa nchini. Ijumaa tumeshuhudia si utekaji nyara au mauaji ya viongozi wa serkali za mitaa, bali limegusa sasa hata jeshi letu la polisi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ombi langu binafsi na ombi la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, katika hatua hii, Serikali itoe tamko kuhusiana na jambo hili ili kuondoa mashaka au mawazo ya watu ambao wanafikiri ukimya huu wa Serikali, na kukataa huku kwa Serikali uchunguzi wa masuala haya usifanyike, yamkini Serikali ndiyo inayoratibu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ruth Hiyob Mollel (Mb)

**WAZIRI KIVULI, NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

18 Aprili, 2017